2 / 2024

# Kutathmini michango ya vibanda, vioski, na mikahawa midogo inayoendeshwa na wanawake katika biashara za chakula jijini Nairobi, Kenya.

**Waandishi:** Christian Sonntag, Emmanuel Atamba, Nicole Paganini, William Onura (TMG Research), Maureen Musya, Evans Otibine, Omondi Okoyo, Patrick Njoroge (Akiba Mashinani Trust, AMT), Jane Masta (Streetnet International), Anthony Kwache (Kenya National Alliance of Street Vendors and Informal Traders, KENASVIT)




Muuzaji katika soko la Wape Wape, Mukuru kwa Njenga, © AMT

## Muhtasari

Mtazamo wa ufeministi na mwingiliano ni muhimu ili kuelewa kikamilifu jukumu muhimu ambalo wanawake hutekeleza katika mfumo wa chakula mijini, hasa katika makazi duni na miongoni mwa maskini. Licha ya nafasi muhimu wanayoshikilia wanawake katika biashara ya chakula isiyo rasmi, wanakumbana na hasara na changamoto nyingi. Ni muhimu kubadili mtazamo, ili kuelewa majukumu mengine muhimu ambayo wafanyabiashara wa chakula wasio rasmi hutekeleza kwa jamii. Hii ndio msingi wa namna ya mbele wa kutoa msaada endelevu na uliolengwa kwa wafanyabiashara wa chakula wasio rasmi. Tunapendekeza kuwe na umakini zaidi juu ya ukandamizaji wa wanawake katika maeneo ya mijini na vijijini kuliko ilivyoelekezwa katika HLPE-FSN Ripoti #19 yenye kichwa "Kuimarisha mifumo ya chakula mijini na pembezoni mwa miji ili kufikia usalama wa chakula na lishe, katika muktadha wa ukuaji wa miji na mabadiliko ya mashambani." Umakini huu unapaswa kujumuishwa zaidi katika mapendekezo ya sera zinazojadiliwa katika CFS 2024. Mapendekezo yetu ya sera yanachukua mbinu ya "kufanya kazi na mfumo usio rasmi" na yanakusudia kuimarisha uundaji wa vyama vya wafanyabiashara wa chakula wasio rasmi, ili kuhakikisha kwamba sauti zao zinasikika na kuanzisha mazungumuzo kati ya rika.

## Utangulizi

Ingawa jamii ya Kenya bila shaka ni inabadilika, inabakia kwa undani mfumo dume. Wanawake wanabaki pembeni katika uongozi wa kisiasa na kwa kiasi kikubwa wametengwa katika kufanya maamuzi katika nyanja za kijamii na kiuchumi (Simiyu, 2018). Wanawake bado huwakilishwa kwa kiwango kidogo katika nafasi za usimamizi na uongozi katika biashara na utawala. Kwa mfano, wao asilimia 24 tu (kada za kazi M hadi P) ya wafanyakazi wa sekta ya umma (Mutuma, 2022).

Ukandamizaji wa kimfumo dhidi ya wanawake unaonekana pia katika mifumo ya chakula ya nchi: Katika maeneo ya vijijini Kenya, wanawake wana jukumu kuu katika kuhakikisha kwamba familia zao sio tu zimeshiba vizuri, bali pia zenye lishe bora licha ya kuwa na uwezo mdogo wa kufanya maamuzi juu ya rasilimali za uzalishaji (HLPE, 2024). Wanawake huchangia hadi asilimia 70 ya wafanyakazi wa kilimo nchini Kenya (Empow'her Global, 2024) na wao kwa kipimo kikubwa wanashikilia maarifa muhimu ya chakula asili lakini bado wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji mdogo wa ardhi ya kilimo na mitaji kwa ajili ya uzalishaji (Brückner, 2020; KIPPRA, 2024). Katika mifumo ya chakula ya mijini, ambapo shughuli kuu ni usambazaji na uuzaji, wanawake wanachukua jukumu muhimu lakini mara nyingi hupuuzwa katika biashara ya chakula isiyo rasmi ambayo inawapatia chakula takriban asilimia 50 ya wateja jijini Nairobi (Tschirley et al. 2010) na

asilimia 90 ya wateja katika makazi yasiyo rasmi kama vile Mukuru (utafiti unaoendelea na AMT na TMG Research).

Kwa upatikanaji mdogo wa fursa katika biashara rasmi ya chakula inayotawaliwa na makampuni makubwa ya rejareja, ya kitaifa na kimataifa, wanawake, hasa katika makazi duni ya mijini wamepata nafasi katika biashara ya chakula isiyo rasmi. Kazi yao ni muhimu kwa kulinda riziki ya kaya na usalama wa jumla wa chakula jijini Nairobi Wafanyabiashara wa chakula wasio rasmi pia wana majukumu kadhaa muhimu zaidi ya kusambaza chakula katika nchi nyingi zenye kipato cha chini na kati, hasa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na Asia Kusini (GAIN, 2020).

Muhtasari huu wa maoni unaonyesha jinsi wafanyabiashara wanawake wa chakula wasio rasmi wanavyokandamizwa kimfumo na mbinu iliyopo ya mfumo wa chakula wa mijini ulio "wa kisasa, rasmi" na unaolenga ukuaji (HLPE, 2024). Maandishi haya yanashiriki mtazamo wa HLPE-FSN Ripoti #19 (2024) kwamba "vipengele vya kitamaduni na visivyo rasmi vya mifumo ya chakula ni muhimu kwa usalama wa chakula na riziki katika mifumo ya chakula ya mijini na pembezoni mwa miji (U-PU) na vinapaswa kuimarishwa". Tunabainisha zaidi kinachoweza kupotea kutokana na kuendelea kwa ukosefu wa msaada na kudhoofika kwa wafanyabiashara wa chakula wasio rasmi kwa upande wa riziki na pia thamani ya ziada inayotolewa na biashara ya chakula isiyo rasmi. Muhtasari huu unakwenda zaidi ya HLPE na unatoa mapendekezo madhubuti ya kuunga mkono sekta ya chakula isiyo rasmi jijini Nairobi na kuunda mazingira ya kuwezesha kwa kuimarisha sauti, uwezo na muundo wa wafanyabiashara wa chakula wasio rasmi. Tofauti na maduka rasmi ya rejareja ya chakula, katika hali nyingi, biashara ya chakula isiyo rasmi ni shughuli ya kujikimu kimaisha badala ya biashara jitahidi. Ni mkakati wa kujikimu unaokuja na changamoto nyingi kama vile upatikanaji mdogo wa mtaji, bei za juu za chakula, ukosefu wa ujuzi wa biashara, miundombinu duni kama vile barabara na mifumo ya kuondoa maji, usimamizi duni wa taka, ukosefu wa vifaa vya kuhifadhi na kupooza chakula, na kukabiliana na hatari za kiafya na usalama, hatua za adhabu, masuala ya usalama na unyanyasaji hasa wakati wa alfajiri na usiku. Programu ya Urban Food Futures ya TMG Research imeunda neno "biashara kwa ajili ya kula" kuelezea shughuli za wafanyabiashara wa chakula wasio rasmi jijini Nairobi (Paganini & Weigelt, 2023). Sekta isiyo rasmi ya chakula kama njia kuu ya upatikanaji wa chakula kwa maskini wa mijini unawakilisha upande mmoja wa maneno "biashara kwa ajili ya kula". Upande wa pili ni kwamba sekta isiyo rasmi hutoa ajira na kipato kwa kaya. Katika masomo ya kesi halisi yetu ya hali halisi katika makazi yasiyo rasmi ya Mukuru jijini Nairobi, zaidi ya theluthi mbili ya wafanyabiashara ni wanawake. Takwimu za mapato ya kaya kwa wafanyibiashara hawa zinaonyesha kuwa uuzaji wa chakula ndio chanzo pekee cha mapato cha kaya kwa wafanyibiashara wengi (utafiti unaoendelea na *AMT/TMG Research*).

Kwa hivyo, hoja zetu kuu kama mchango kwa mijadala ya CFS ya mwaka huu ili kuimarisha Mifumo ya Chakula ya Mijini na Pembezoni mwa Miji ni:

- Kutumia mtazamo wa ufeministi na mwingiliano kuelewa michango ya wanawake katika mfumo wa chakula wa kina, jumuishi na wenye ustahimilivu unaozidi ugavi wa chakula.
- "Kufanya kazi na mfumo usio rasmi" kama mbinu ya uendelevu wa kiuchumi na kijamii katika mifumo ya chakula.
- Kuimarisha sekta ya chakula isiyo rasmi kwa mashirika kama vyama vilivyojengwa kwa mitandao ya kijamii ndani ya jamii vinahitaji mazingira wezeshi yanayotolewa na serikali.



Mchuuzi katika Mukuru Kwa Njenga, © AMT

## Fikra ya kuzingatia zaidi ya HLPE

Soko la chakula lisilo rasmi linachukuliwa kuwa halina ufanisi na halijaandaliwa vizuri, na mara nyingi linahusishwa moja kwa moja na chakula kisicho salama, na linaonekana kama kinyume cha masoko ya chakula rasmi (Racaud et al., 2018). Ingawa HLPE-FSN Ripoti #19 inajadili jukumu muhimu na kazi za wafanyabiashara wa chakula wasio rasmi,

haielezei kwa mtazamo wa ufeministi. Ripoti ya HLPE inasema kwamba wafanyabiashara wa chakula wasio rasmi "wanakidhi mahitaji ya wateja wa kipato cha chini kwa kuuza kwa viwango vidogo, kutoa mikopo, na mara nyingi kufanya kazi kwa muda mrefu ili kukidhi mahitaji ya wasafiri wa mijini" (HLPE, 2024, uk. 64) na wafanyabiashara isiyo rasmi "wanauza vyakula vya kitamaduni vinavyokubalika kijamii" (HLPE, 2024, uk. 47). Umuhimu wa wanawake katika biashara ya chakula isiyo rasmi pia unajadiliwa (HLPE 2024, uk. 34).

Hata hivyo, ripoti hiyo haina mtazamo thabiti wa ufeministi na mwingiliano kuhusu ukandamizaji wa kimfumo na usawa wa kijinsia katika muktadha wa biashara isiyo rasmi. Kwa hivyo, uchambuzi na msisitizo wa michango mingine muhimu kando na ugavi wa chakula, hasa zinazotolewa na wanawake katika mfumo wa chakula wa mijini, unakosa kina. Wanawake ni uti wa mgongo muhimu wa mfumo wa chakula wa mijini na wanapaswa kupewa msaada zaidi.

Ili kutoa mfano halisi wa hili, maandishi yetu yanapanua mada hii, kuongeza uzito, na kutoa data za sasa na thabiti pamoja na mapendekezo madhubuti yanayotokana na utafiti wa hatua kuhusu kuanzishwa kwa Chama cha Wafanyabiashara wa Chakula katika makazi yasiyo rasmi ya Mukuru, Nairobi.

Wakati wa urasimishaji na uboreshaji wa sekta ya chakula, wanawake mara nyingi wanasalia nyuma kwani kazi zenye ujira mzuri na ujuzi zaidi hupewa wanaume. Mtanziko huu umeonyeshwa na Muungano wa Kimataifa wa Kuboresha Lishe (GAIN):

»Katika nchi nyingi, kanunu za kijinsia zenye ubaguzi zinawazuia wanawake kupata fursa za kujipatia kipato zinazotolewa na miji, na hivyo hupunguza usalama wa chakula kwao na kwa familia zao. Matokeo yake, wanawake mara nyingi hulazimika kufanya kazi katika njia zisizo rasmi za kujipatia riziki, mara nyingi kama wafanyabiashara wa chakula, wakitegemea mitandao ya kijamii kupata chakula na pesa. Na masoko haya yasiyo rasmi mara nyingi hupuuzwa na wapangaji wa miji«

Utafiti na GAIN, katika Morris & Mbuya, 2024.

Miradi mingi inayolenga kuboresha maisha ya wanawake katika nchi zinazoendelea huwa inalenga zaidi haki za msingi za wanawake na vipengele vya usalama kama vile kuondoa unyanyasaji wa majumbani. Kuunga mkono fursa za kiuchumi za wanawake' inapaswa kuwa kipaumbele cha juu pia (HLPE, 2024, uk. 34). Mtazamo hasi dhidi ya biashara ya chakula isiyo rasmi unachangia zaidi kupunguza nafasi, ambayo tayari ni ndogo, ya wanawake katika usambazaji wa chakula. Kadiri sera za kimataifa za chakula zinavyozidi kuelekea kushughulikia mahitaji ya wateja yanayoongezeka kuhusu ubora wa chakula, ufuatiliaji, usalama na uhakikisho wa ubora, biashara ya chakula isiyo rasmi inapuuzwa na watunga sera au kuchukuliwa kama kizuizi.



Mkutano wa Kikundi cha Wachuuzi Mukuru Safina Fresh katika Mukuru Kwa Njenga, © AMT

Mwaka wa 2012, Shirika la *Women in Informal Employment: Globalizing and Organizing* (WIEGO) lilifanya utafiti wa "Informal Economy Monitoring Study (IEMS)" katika miji ya Accra (Ghana), Ahmedabad (India), Bangkok (Thailand), Belo Horizonte (Brazil), Bogota (Colombia), Durban (Afrika Kusini), Lahore (Pakistan), Lima (Peru), Nakuru (Kenya) na Pune (India). Utafiti huo (WIEGO, 2024) ulifichua jinsi wafanyabiashara wa sekta isiyo rasmi wanavyoimarisha jamii zao kwa kutoa chanzo kikuu cha mapato ya kaya nyingi. Sekta isiyo rasmi ina uhusiano wa nguvu na uchumi rasmi kwani wafanyabiashara wengi wanajaribu kusafisha barabara na kuboresha usalama wa wateja wao na kuwashughulikia wateja kwa huduma ya kibinafsi na yenye urafiki. Uundaji wa ajira (k.v. wapagazi, walinzi, waendeshaji wa usafiri, watoa huduma za kuhifadhi) na uzalishaji wa mapato (k.v. malipo ya leseni, vibali, ada, faini na kodi) ni michango mingine inayotolewa na baadhi ya wafanyabiashara wa sekta isiyo rasmi. Mwisho lakini si kwa uchache, biashara isiyo rasmi mara nyingi "pia inaongeza uhai katika maisha ya mijini na katika maeneo mengi inachukuliwa kuwa nguzo ya urithi wa kihistoria na kitamaduni" (WIEGO, 2024).

Licha ya michango yao, wafanyabiashara wanakumbana na changamoto nyingi na mara nyingi hupuuzwa kama mawakala wa kiuchumi. Tofauti na biashara nyingine, ambapo mara nyingi wanasahaulika na kuzuiwa badala ya kusaidiwa na sera na taratibu za manispaa.

## Kutoka kwenye somo la kesi halisi hadi CFS (Kutoka Mukuru hadi Ulimwengu)

Katikati ya eneo la viwanda la Nairobi, makazi yasiyo rasmi ya Mukuru yana eneo la hekta 280 na yanajumuisha vijiji sita. Tangu miaka ya 1980, Mukuru, kama makazi mengi yasiyo rasmi ya Nairobi, imekua kwa kasi na bila mipango rasmi kutokana na umaskini, ukuaji wa kasi wa miji, mipango mibovu ya miji, na usimamizi wa rasilimali za ardhi uliojaa ufisadi (Mutinda et al., 2020). Leo, Mukuru ni makazi ya zaidi ya kaya 100,000 (Lines et al., 2020) na ina uchumi wenye nguvu usio rasmi. Ingawa yanachukua chini ya asilimia 5 ya eneo la makazi ya jiji, makazi yasiyo rasmi kama Mukuru yanakaliwa na zaidi ya asilimia 60 ya wakazi wa Nairobi (Mallory et al., 2020). Wingi wa watu unasababisha changamoto kubwa za usafi, ambapo idadi kubwa ya wakazi wapatao 300,000 wanashiriki vyoo vya shimo 3,863 pekee (Njoroge & Musya, 2021). Huduma za umma kama vile umeme, maji, na usimamizi wa taka ni haba. Kutokuwepo kwa msaada wa serikali, mapengo haya yamenyakuliwa haraka na watoa huduma zisizo rasmi na magenge yanayojinufaisha kutokana na ukosefu wa huduma za serikali. Wakati huduma hizi zinatoa ajira kwa wengi, zinabebesha wakazi wa Mukuru mzigo wa kodi, na zimeelezewa na AMT/Muungano kama adhabu ya umaskini inayozuia ustawi wa wakazi, ikijumuisha usambazaji wa umeme usio salama na usambazaji wa maji usio salama na usiotosheleza (Mutinda et al., 2020).

Katika Nairobi, kama ilivyo katika miji mingi ya Kusini mwa Dunia, sehemu kubwa ya biashara za chakula isiyo rasmi ni mbinu ya kujikimu kwa kaya maskini [zaidi ya asilimia 70 ya wafanyabiashara waliohojiwa wana kipato hiki pekee cha kaya (Utafiti unaoendelea wa AMT/TMG Research)]. Tofauti na minyororo rasmi ya ugavi wa chakula, biashara ya chakula isiyo rasmi inatawaliwa na wanawake. Utafiti uliofanywa na *Akiba Mashinani Trust* na *TMG Research* unakadiria kwamba asilimia 74 ya wafanyabiashara wa chakula wasio rasmi katika makazi ya Mukuru ni wanawake. Hiyo kwa kiasi fulani inatokana na ukosefu wa njia mbadala za kupata mapato. Kazi zenye ujira mzuri ziko nje ya makazi yasiyo rasmi, mara nyingi katika viwanda kwenye maeneo ya viwanda au kama wahudumu katika maeneo ya kituo cha biashara cha kati ya mji au kwenye mahoteli karibu na Uwanja wa Ndege au kwenye maeneo ya kiwango cha juu Kaskazini na Magharibi mwa jiji, ambazo



Wanawake wakitayarisha chakula huko Mukuru, Nairobi, © AMT

mara nyingi si rahisi kufikiwa na wanawake. Kinachobakia kwa wanawake katika maeneo ya makazi yasiyo rasmi ni shughuli kama vile uuzaji (wa chakula) katika maeneo hayo.

Licha ya changamoto nyingi, sekta isiyo rasmi ni muhimu katika kuwapatia chakula jamii masikini za mijini. Wafanyabiashara wasio rasmi huchukua majukumu muhimu ya uendeshaji wa mwisho na kazi za rejareja ndani ya makazi yasiyo rasmi. Tschirley et al. (2010) wanakadiria kwamba zaidi ya asilimia 50 ya ununuzi wa chakula jijini Nairobi hufanywa kutoka kwa wafanyabiashara wasio rasmi, huku kaya maskini kutoka makazi yasiyo rasmi zikiwa kundi kubwa zaidi la wateja. Zaidi ya asilimia 90 ya kaya katika Mukuru zinatumia soko la chakula lisilo rasmi kununua bidhaa za chakula (utafiti unaoendelea wa *AMT* & *TMG Research*).

Uchunguzi wetu kifani/utafiti wa hatua shirikishi pamoja na wachuuzi wa vyakula wasio rasmi huko Mukuru ilibainika kuwa uuzaji wa chakula usio rasmi hutoa huduma nyingi za ziada zaidi ya chakula wanachouza. Hii inajumuisha kutoa chakula kwa mkopo kwa wateja wao, kutoa vyakula vilivyopikwa tayari na hivyo basi kupunguza gharama za nishati kwa chakula kama nafaka, na kutoa huduma za uangalizi wa watoto na ushauri kuhusu lishe kwa wanawake, vijana na watoto. Kwa bahati mbaya, huduma hizi muhimu na za ziada zinazotolewa na biashara za chakula zinazoendeshwa na wanawake hazitambuliwi na serikali za mitaa wala kitaifa pamoja na wadau wengine. Kinyume chake, biashara ya chakula isiyo rasmi inaendelea kulaumiwa na kushutumiwa kuwa si salama na hatari, huku ikikabiliana na changamoto nyingi kama vile upatikanaji mdogo wa mitaji, bei za juu za chakula, ujuzi wa biashara usiotosha, miundombinu duni, usimamizi mbovu wa taka Kwa bahati mbaya, huduma hizi muhimu za ziada hazitambuliwi na serikali za mitaa na kitaifa na wadau wengine. Kinyume chake, uuzaji wa

chakula usio rasmi unaendelea kuharibiwa sifa kwamba siyo salama.

Vibanda vya soko vya chakula vinavyoendeshwa na wanawake, vioski na mikahawa katika makazi yasiyo rasmi hutoa zaidi ya chakula na kipato tu kwani lakini pia hutoa huduma za kipekee za kitamaduni na kijamii. Makazi yasiyo rasmi ya Nairobi, yenye watu wengi wenye asili mbalimbali kutoka mikoa yote ya Kenya na nje ya nchi, yanaathiri tabia kuhusu chakula na lishe (HLPE, 2024). Maarifa na uzoefu kuhusu vyakula na mapishi tofauti hushirikishwa katika vibanda vya chakula visivyo rasmi na mikahawa. Wanatoa njia za kushiriki na kubadilishana maarifa kuhusu aina mbalimbali za vyakula, mapishi, na lishe. Wafanyabiashara wasio rasmi pia hutoa chakula kwa vipande kulingana na mahitaji ya kaya/matumizi ya wateja, kupika nafaka kabla ya kuuza na kutoa chakula kwa mkopo kwa wateja wao walioko katika hali ngumu kifedha na katika dharura. Pia ni chanzo muhimu cha chakula kilichopikwa kwa idadi kubwa ya wakazi maskini katika makazi yasiyo rasmi, ambao hawana vifaa wala njia za kuandaa chakula chao wenyewe.

Utawala wa wanawake katika biashara ya chakula isiyo rasmi umefanya vibanda vya mboga yawe na jina 'mama mboga', jina linalomaanisha mwanamke wa mboga. Pia ni kawaida Nairobi kuwaita wanawake wanaoendesha vibanda vya chakula, mara nyingi visivyo rasmi, 'kwa mathe' ambayo ina maana mahali pa mama. Majina haya ni ushahidi wa heshima kubwa wanayopewa wanawake wanaoendesha biashara za chakula na wateja. Kuuza karibu na nyumbani pia kuna faida kubwa kwa wafanyabiashara wanawake kwani gharama za malezi ya watoto na usafiri ni za chini; wanaweza kuchanganya vizuri shughuli zao za kujikimu na kazi za nyumbani (Sverdlik, 2016). Kwa upande mwingine, wanawake wanakumbana na changamoto za kiusalama karibu na masoko wanaponunua bidhaa usiku na wanakabiliwa na vurugu na unyanyasaji, jambo lililotajwa na wafanyabiashara wanawake wote waliohojiwa (Utafiti wa *AMT/TMG*, 2024).

## (Sera) Mapendekezo

- Kutumia **mtazamo wa ufeministi na mwingiliano** kuelewa michango wanawake hutoa kwa mfumo wa chakula unaojumuisha na ustahimilivu zaidi ya usambazaji wa chakula.
- Tambua wachuuzi wa chakula wasio rasmi kama sehemu ya suluhisho la uhaba wa chakula kwa watu maskini wa mijini na hivyo kutetea mbinu ya "Kufanya kazi kwa njia isiyo rasmi" (Vorley, 2023).
- Kuimarisha sauti na shirika la wafanyabiashara wa chakula wasio rasmi kwa kuanzisha **vyama vya wafanyabiashara wa chakula** kulingana na mitandao iliyoanzishwa ndani ya jamii kunahitaji mazingira wezeshi yanayotolewa na serikali.
- Tunatetea kuhusu "kukuza mamlaka na uwezo wa wanawake nani ya mifumo ya chakula" na yatakayonufaisha wote — "hiyo ina maana kwamba wanaume lazima wachukue hatua" (Morris & Mbuya, 2024).

## Hitimisho

Wanawake bado wanakabiliwa na upatikanaji mdogo wa rasilimali, miundombinu, na ufikiaji mdogo wa majukwaa ya kufanya maamuzi katika mifumo ya chakula, ingawa wanawake ni sehemu muhimu ya mifumo ya chakula, kuanzia kupanda mbegu hadi kuandaa masoko (yasiyo rasmi), lakini mara nyingi hupuuzwa (Morris & Mbuya, 2024). Kupuuza kimfumo majukumu muhimu ya wanawake pamoja na changamoto wanazokabiliana nazo katika biashara ya chakula isiyo rasmi kunachangia ukandamizaji wa kimfumo, kupitia sera zisizo za kuunga mkono, sheria ndogo ndogo zinazokandamiza, na mifumo ya kifedha inayowatenga. Ingawa biashara ya chakula isiyo rasmi inakumbana na changamoto za kushughulikia uhaba wa miundombinu, bado ni nguzo kuu katika mfumo wa chakula wa mijini.

## Kuhusu

Urban Food Futures ni programu ya "Sayansi na Jamii". Ikiwa na vituo Nairobi na Cape Town, utafiti wetu unalenga makazi yasiyo rasmi na vitongoji vya mijini vya kipato cha chini ambavyo kwa kiasi kikubwa vimefungiwa nje ya utoaji rasmi wa huduma na miundo ya utawala. Kwa kutumia hali isiyo rasmi kama kiunganishi, tunachunguza njia za kubadilisha mifumo ya chakula na kufanikisha haki ya chakula kwa wote.

# Marejeleo


Brückner, M. (2020). Learning degrowth from women's food knowledge and care in Kenya. In A. Nelson & F. Edwards, *Food for Degrowth: Perspectives and Practices.* Routledge.

Empow'her Global (2024). *Gender dynamics in Kenyan coffee production.* https://empow-her.com/en/gender-dynamics-in-kenyan-coffee-production/

GAIN (2020). *Informal food retail in urban areas. Factsheet. Urban Governance for nutrition programme.* The Global Alliance for Improved Nutrition. https://www.gainhealth.org/sites/default/files/publications/documents/informal-food-retail-in-urban-areas.pdf

HLPE (2024). *Strengthening urban and peri-urban food systems to achieve food security and nutrition, in the context of urbanization and rural transformation.* CFS HLPE-FSN.

KIPPRA. (2024). *Promoting Land Ownership among Women in Kenya.* Kenya Institute of Public Policy Research and Analysis. https://kippra.or.ke/promoting-land-ownership-among-women-in-kenya/#:~:text=The%202022%20KDHS%20report%20reveals,own%20any%20land%20in%20Kenya.

Lines, K., Mitlin, D., Mwelu, J., Njenga Maina, J. P., Okoyo, O., Otibine, E., Wakesho, T., & Kiarie, M. A. W. (2020). *Bridging the affordability gap: Towards a financing mechanism for slum upgrading at scale in Nairobi analysing NGO experiences with local-level finance: Vol. GDI Working Paper 2020-042.* The University of Manchester. http://hummedia.manchester.ac.uk/institutes/gdi/publications/workingpapers/GDI/GDI-working-paper-202042-Lines-Mitlin.pdf

Mallory, A., Omoga, L., Kiogora, D., Riungu, J., Kagendi, D., & Parker, A. (2020). Understanding the role of informal pit emptiers in sanitation in Nairobi through case studies in Mukuru and Kibera settlements. *Journal of Water, Sanitation and Hygiene for Development*, 11(1), 51–59. https://doi.org/10.2166/washdev.2020.193

Morris, S., & Mbuya, M. (2024). Women are central to global food systems–Men must recognize and act upon that. *World Economic Forum. Gender Inequality.* https://www.weforum.org/agenda/2024/03/women-integral-global-food-systems-men-must-recognize-and-act-upon-that/

Muli, J. (2023). Women Smallholders Will Drive Africa's Transition to Regenerative Agriculture. *Business Fights Poverty.* https://businessfightspoverty.org/women-smallholders-will-drive-africas-transition-to-regenerative-agriculture/

Mutinda, M., Mwau, B., Makau, J., & Sverdlik, A. (2020, May 1). Policy briefing: Rethinking slum upgrading in light of Nairobi's poverty penalty (SDI Kenya). *Muungano Wa Wanavijiji.* https://www.muungano.net/publicationslibrary/2020/5/20/muungano-alliance-policy-briefing-rethinking-slum-upgrading-in-light-of-nairobis-poverty-penalty

Mutuma, S. (2022). *Womens's participation in management and leadership positions in the public service in Kenya: Closing the gender gap* (Women's Economic Empowerment Hub.). Kenyatta University.

Njoroge, P., & Musya, M. (2021, December 21). Stories of Change: Mukuru Water and Sanitation pilot project update. *Muungano Wa Wanavijiji.* https://www.muungano.net/browseblogs/2022/1/7/story-of-change-mukuru-water-and-sanitation-pilot-project-update

Owuor, S., Brown, A., Frayne, B., & Wagner, J. (2017). *The Urban Food System of Nairobi*, Kenya (6; Hungry Cities Partnership, p. 79).

Paganini, N., & Weigelt, J. (2023). *Pathways to Transform Urban Food Systems: Progressively Realising the Right to Food through a Strengthen Informal Sector in Cape Town and Nairobi.* TMG Research gGmbH. https://doi.org//10.13140/RG.2.2.23410.17602/1

Racaud, S., Kago, J., & Owuor, S. (2018). Introduction: Contested Street: Informal Street Vending and its Contradictions. *Articulo – Revue de Sciences Humaines*, 17–18. https://doi.org/10.4000/articulo.3719

Simiyu, S. (2018). GENDER: 12th Parliament shows Kenya deeply patriarchal. *International Commision of Jurists (ICJ). Kenya Section.* https://icj-kenya.org/news/gender-12th-parliament-shows-kenya-deeply-patriarchal/

Sverdlik, A. (2016). Nourishing livelihoods: The food vendors sustaining Nairobi's slums. *IIED.* https://www.iied.org/nourishing-livelihoods-food-vendors-sustaining-nairobis-slums

Tschirley, D., Ayieko, M., Hichaambwa, M., Goeb, J., & Loescher, W. (2010). *Modernizing Africa's Fresh Produce Supply Chains Without Rapid Supermarket Takeover: Towards a Definition of Research and Investment Priorities.* (93030; Food Security International Development Working Papers). Michigan State University, Department of Agricultural, Food, and Resource Economics.

Vorley, B. (2023). *Working with informality: Constructive ways to transform food systems.* IIED and SNV.

WIEGO (2024). *Street vendors and the law.* Women in Informal Employment: Globalizing and Organizing. https://www.wiego.org/street-vendors-and-law



Kwa ushirikiano na

Uchapishaji huu umewezekana kwa msaada wa kifedha kutoka kwa German Federal Ministry.

Federal Ministry for Economic Cooperation and Development



TMG Research

TMG – Think Tank for Sustainability
TMG Research gGmbH
EUREF-Campus 6–9
10829 Berlin, Germany
Phone: +49 30 92 10 74 07 00
Email: info@tmg-thinktank.com
Website: www.tmg-thinktank.com